HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 020 | OKTOBA - DISEMBA, 2025

# NEMC YACHOTA HAZINA KUBWA YA NAMNA YA KUHIFADHI NA KUSIMAMIA MAZINGIRA KUTOKA KWA DKT. MPANGO




**Ndani:**

- NEMC YAKUTANA NA MAKAMU WA RAIS MHE. BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI DODOMA
- NEMC YAHAMASISHA USAFI WA MAZINGIRA SHIMUTA 2025 – MOROGORO
- NEMC YASHIRIKI UNFCCC COP-30, BELEM, NCHINI BRAZIL


@nemctanzania NemcTVTanzania

#MazingiraYetuUhaiWetu

www.nemc.or.tz

# YALIYOMO


1. NEMC YAKUTANA NA MAKAMU WA RAIS MHE. BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI DODOMA ..... 03
2. NEMC YACHOTA HAZINA KUBWA YA NAMNA YA KUHIFADHI NA KUSIMAMIA MAZINGIRA KUTOKA KWA DKT. MPANGO ..... 04
3. NEMC YAWALETA PAMOJA WATUMISHI WAKE KUJIPANGA KWA MWAKA 2026 ..... 05
4. NEMC NA ZEMA ZAIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ..... 06
5. ELIMU YA MAZINGIRA YATOLEWA KWA WANAFUNZI, WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA ..... 07
6. NEMC KANDA YA KATI YATOA MAFUNZO KWA WAKANDARASI WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA ..... 07
7. NEMC NA ZEMA ZAKUBALIANA KATIKA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA NCHINI ..... 08
8. NEMC YASHIRIKI KONGAMANO JUU YA UHIFADHI WA BAHARI YA HINDI ..... 09
9. NEMC KANDA YA BAGAMOYO YATOA ELIMU YA MAZINGIRA SHULE YA MSINGI NIA NJEMA ..... 10
10. NEMC YAWAFIKIA MAAFISA WA FORODHA MIPAKANI - ELIMU YA MAZINGIRA ..... 11
11. NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA KIMATAIFA WA TAKA ZA KIELEKTRONIKI NCHINI KENYA ..... 12
12. NEMC YASHIRIKI KIKAO CHA TEKNOLOJIA ZA UREJESHAJI MAZINGIRA NCHINI AUSTRIA ..... 13
13. NEMC NA EU YAJADILI MASUALA YA KIMAZINGIRA SEKTA YA MADINI ..... 13
14. NEMC YAWANOA MAAFISA FORODHA KIGOMA - ELIMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA ..... 14
15. NEMC NA IUCN KUKABILIANA NA TATIZO LA UCHAFUZI WA TAKA ZA PLASTIKI UKANDA WA BAHARI ..... 15
16. MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI NA ATHARI ZAKE KWA UBORA WA MAJI KATIKA SEHEMU YA CHINI YA MTO MARA, TANZANIA ..... 15
17. NEMC YAHITIMISHA MAFUNZO KWA MAAFISA FORODHA – ELIMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA TUNDUMA ..... 16
18. KAMISHNA TUME YA UTUMISHI WA UMMA AIPONGEZA NEMC KWA UADILIFU KATIKA UTUMISHI WA UMMA ..... 17
19. NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA BIOANUAI, PANAMA 2025 ..... 18
20. NEMC YAJINASIBU KUFANYA MAKUBWA SHIMMUTA 2025, YAPOKEA VIFAA KUTOKA MRADI WA ADAPTATION FUND ..... 19
21. NEMC KANDA YA MAGHARIBI YAPATA MAFUNZO YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA ..... 20
22. NEMC YAADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA KWA VITENDO ..... 20
23. NEMC YASHIRIKI KIKAO KAZI KUHUSU AKILI MNEMBA NA MASOKO YA KIDIGITALI ..... 21
24. NEMC YAENDESHA MAFUNZO YA NDANI JUU YA MCHAKATO WA KUPITIA MIRADI YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA ..... 22
25. NEMC YASHIRIKI UNFCCC COP-30, BELEM, NCHINI BRAZIL ..... 23
26. NEMC YAENDESHA MAFUNZO YA NDANI JUU YA MAPITIO YA TAARIFA ZA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA JAMII NA KAGUZI ZA MAZINGIRA ..... 24
27. NEMC YAPATA MAFUNZO YA UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2050 ..... 25
28. NEMC YAELIMISHA UMMA UDHIBITI WA KELELE CHAFUZI NA MITETEMO ..... 26
29. NEMC YAILAZA WCF 5 BILA SHIMMUTA 2025 ..... 27
30. DKT. FESTO DUGANGE AZUNGUMZA NA WATUMISHI WA NEMC ..... 28
31. NEMC YAENDESHA MAFUNZO KUHUSU NYENZO ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA WIZARA, TAASISI NA HALMASHAURI ZA MANISPAA NA WILAYA ..... 29
32. NEMC YASAINI MAKUBALIANO YA AWALI NA UPS KUANZISHA MFUMO WA KIDIGITALI WA UFUATILIAJI WA UCHAFUZI WA MAZINGIRA ..... 30
33. NEMC YAENZI MAADHIMISHO YA SIKU YA WALEMAVU DUNIANI ..... 31
34. NEMC YAHAMASISHA USAFI WA MAZINGIRA SHIMMUTA 2025 - MOROGORO ..... 32
35. NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA SABA WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU MAZINGIRA ..... 33
36. KAULI YA MAZINGIRA YETU ..... 34

## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria hiyo Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira; na
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
**Dkt. Menan Jangu**

**Mhariri Mkuu:**
**Martha P. Kawishe**

**Wachangiaji:**
Boniphace Kyaruzi
Tajiri Kihembla
Aziza Muhali
Catherine Ngowi
Alpha Ndahoze
Mary Ntupwa

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# NEMC YAKUTANA NA MAKAMU WA RAIS MHE. BALOZI DKT. EMMANUEL JOHN NCHIMBI DODOMA

Ni katika kikao kazi cha kupitishana kwenye majukumu ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi akizungumza na Watendaji wa Ofisi zilizopo chini ya Ofisi yake wakiwemo NEMC katika kikao kazi cha kwanza tangu kuteuliwa kwake chenye lengo la kupitishana kwenye majukumu ya utekelezaji wa Taasisi hizo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikutana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwenye kikao kazi cha kwanza na watendaji wake tangu kuteuliwa kwake chenye lengo la kupitishana kwenye majukumu ya utekelezaji wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi yake.

Kikao hicho kilichofanyika katika ukumbi wa Hazina jijini Dodoma kilihusisha Menejimenti na watumishi kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais, Menejimenti ya Baraza pamoja na watendaji kutoka kituo cha Taifa cha Ufuatiliaji wa masuala ya Kaboni.

Akizungumza katika kikao hicho Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi alisema ni kikao cha kukumbushana wajibu tulionao kwa watanzania wa kudumisha Muungano pamoja na kusimamia masuala mazima ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini hasa ikizingatiwa dira ya maendeleo ya 2050 kipengele cha tatu kimezingatia masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira pamoja na Ustahimilivu wa masuala mazima ya mabadiliko ya Tabianchi.

"Dhamana tuliyopewa ni kubwa, masuala ya Muungano, kutunza mazingira na uchumi wa buluu si vitu vya mchezo, ni lazima tumsaidie Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya siku mia moja (100) kutekeleza maagizo yahusuyo Muungano na Mazingira, tunao wajibu wa kuhakikisha Mazingira yanasimamiwa na kuhifadhiwa" Amesema Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi.

Alitoa maagizo yafuatayo: kila mtumishi aisome ilani ya chama kilichopo madarakani pamoja na dira ya maendeleo ya 2050 kwani ndio msingi wa utekelezaji wa majukumu ya Serikali, masuala ya Muungano na Mazingira, Uchumi wa buluu, biashara ya kaboni na nishati safi yasimamiwe na kutekelezwa kwa weledi, malengo yote ya utekelezaji wa shughuli za Muungano na Mazingira yawe na namna sahihi ya ufuatiliaji na utekelezaji wake ili kufikia azma iliyokubaliwa.

Maagizo mengine ni kuandaa mkakati wa mawasiliano utakaotoa muongozo wa namna ya kutangaza shughuli za mazingira, kuzingatia haki na stahiki za watumishi, kuhakikisha vijana wanaelewa maana halisi ya Muungano na kuuenzi pamoja na wakuu wa Taasisi kusimamia Sheria na Miongozo katika utekelezaji wa majukumu yao.

Awali akimkaribisha Makamu wa Rais, Waziri wa nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Mhandisi Hamad Yussuf Masauni alisema NEMC inahitaji kupewa meno kwani kero za Mazingira zimekuwa nyingi hasa uchafuzi wa vyanzo vya maji na kelele chafuzi za Mazingira.

"Hakuna kitu kinanikera kama pale ocean road kila nikipita napakuta pachafu, panatoa harufu, matakataka yamezagaa, nikiwauliza NEMC wanasema hawana meno" Mhe. Mhandisi Hamad Masauni.

Naye Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Mhandisi Cyprian Luhemeja alipozungumza aliahidi kuyasimamia na kuyatekeleza maagizo na maelekezo yote yaliyotolewa kwa kushirikiana na watendaji wa Taasisi zote zilizo chini ya ofisi ya Makamu wa Rais.

Kikao kazi hicho kilihudhuriwa pia na Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira) Profesa Peter Msoffe na Naibu Katibu Mkuu (Muungano) Bw. Abdallah H. Mitawi.

# NEMC YACHOTA HAZINA KUBWA YA NAMNA YA KUHIFADHI NA KUSIMAMIA MAZINGIRA KUTOKA KWA DKT. MPANGO

## Yachota hazina kubwa ya namna ya kuhifadhi na kusimamia mazingira nchini.




*Makamu wa Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango (wa nne kutoka kulia) akipokea zawadi ya picha kutoka kwa timu ya NEMC iliyomtembelea nyumbani kwake Mayamaya jijini Dodoma ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi (wa tatu kulia mstari wa mbele).*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Novemba 11, 2025 lilifanya ziara maalum nyumbani kwa Makamu wa Rais mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, eneo la Mayamaya mkoani Dodoma, ambapo mazungumzo yenye tija kubwa kuhusu hali ya mazingira nchini yalifanyika.

Katika mazungumzo hayo, Dkt. Mpango alielezea kwa kina wasiwasi wake kuhusu kasi ya uharibifu wa mazingira unaoendelea kushamiri nchini, huku akisisitiza haja ya kuwepo kwa msukumo mkubwa zaidi katika kulinda maeneo ya hifadhi na kusimamia matumizi bora ya ardhi.

Alisema kuwa maeneo mengi ya hifadhi yamekuwa yakivamiwa, mito mingi imechepushwa kinyume na taratibu, huku mabwawa ya kuzalisha umeme yakikumbwa na uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu. Vilevile, biashara ya mbao na mkaa imeendelea kuchangia ongezeko la ukataji miti na hivyo kuongeza kasi ya uharibifu wa misitu nchini.

Dkt. Mpango alibainisha kuwa changamoto za mifugo isiyo na utaratibu mzuri, uchimbaji holela wa mashamba, pamoja na tatizo la mimea vamizi, vinahitaji mikakati madhubuti ya kitaifa. Alisisitiza kuwa NEMC inapaswa kupewa nguvu zaidi katika utekelezaji wa Sheria na Kanuni za mazingira, akisema: "Sauti ya NEMC isiwe tena sauti ya mtu aliye nyikani."

Aidha, Dkt. Mpango alitoa wito kwa Serikali na jamii kwa ujumla kutekeleza kwa vitendo mpango wa Kijanisha mazingira "Greening the Environment", huku akipendekeza kuanzishwa kwa green parks na botanical gardens katika Majiji na Miji mikuu ya nchi, kama sehemu ya kujenga miji yenye mazingira rafiki na yenye afya.

"Ni lazima tujiulize kama Taifa, kama miji, tumechukua hatua gani za kulinda na kurejesha uoto wa asili? Inawezekana kabisa kuwa na mazingira mazuri kama tukidhibiti shughuli zetu kwa kufuata sheria na mipango tuliyojiwekea," alisisitiza Dkt. Mpango.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alipozungumza alipongeza maono na ushauri uliotolewa na Dkt. Mpango, huku akiahidi kuendelea kutumia maarifa hayo katika kuimarisha juhudi za Hifadhi na Usimamizi endelevu wa mazingira nchini.

Ziara hiyo iliyofanywa na Menejimenti ya Baraza imekuwa ni ya muhimu katika kujenga mashirikiano kati ya Taasisi za Serikali na viongozi wastaafu wenye uzoefu mkubwa, kwa lengo la kuhakikisha Tanzania inabaki kuwa nchi yenye mazingira safi, salama, na yenye uendelevu wa kiikolojia.



*Makamu wa Rais Mstaafu Dkt. Philip Isdor Mpango (Katikati) akipokea zawadi kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (kushoto) wakati timu ya NEMC ilipomtembelea nyumbani kwake Mayamaya jijini Dodoma. Kulia ni Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira (NEMC) Dkt. Menan Jangu.*

# NEMC YAWALETA PAMOJA WATUMISHI WAKE KUJIPANGA KWA MWAKA 2026

## Ni katika kufanya tathmini na kuimarisha umoja.

Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Makao Makuu na kutoka kanda zote 13 nchini, walikutana katika eneo la Ndotopolepole, Wilaya ya Bagamoyo, katika hafla maalum iliyolenga kuimarisha mshikamano, kujengeana uelewa, kufanya tathmini fupi ya utendaji kazi na kufurahi pamoja, ikiwa pia ni sehemu ya kufunga mwaka 2025.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, aliwataka watumishi wa Baraza kudumisha umoja na mshikamano katika utendaji kazi (team building), kufanya kazi kwa bidii na kuongeza nidhamu pamoja na unadhifu wa kazi, kama nguzo muhimu za kufanikisha maono na dira ya Taasisi katika mwaka 2026.

Dkt. Semesi aliongeza kuwa katika kuboresha mazingira ya utendaji kazi, NEMC imejipanga kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidigitali, ambapo tayari baadhi ya mifumo ya ufuatiliaji wa mazingira imeanza kutumika, hatua inayolenga kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika kazi.



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi akipokea zawadi ya sanaa ya picha kutoka kwa kamati ya maandalizi ya hafla hiyo iliyofanyika Disemba 19, 2025 eneo la Ndotopolepole Wilayani Bagamoyo.*

Hafla hiyo pia ilihusisha utoaji wa zawadi kwa watumishi walioonesha utendaji kazi mzuri na bidii, ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha ari, nidhamu na ushindani chanya mahali pa kazi.

Akitoa pongezi kwa wafanyakazi waliofanya vizuri, Dkt. Semesi aliipongeza menejimenti na watumishi wote wa NEMC kwa ujumla, na kuwasihi kuongeza bidii, ubunifu na ari mpya katika kutekeleza majukumu yao kwa mwaka 2026.

Aidha, hafla hiyo ilipambwa na michezo mbalimbali ya kujenga ushirikiano, mshikamano na moyo wa kutokata tamaa katika kazi, ambapo washindi walitunukiwa zawadi kama motisha.



*Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) makao makuu Pamoja na wa Kanda zote 13 nchini wakiwa katika picha ya pamoja katika hafla ya iliyowakutanisha pamoja eneo la Ndotopolepole, Disemba 19, 2025.*

# NEMC NA ZEMA ZAIMARISHA USHIRIKIANO KATIKA UHIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA




*Pichani ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (Kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa ZEMA Bw. Sheha Mjaja Juma mara baada ya kikao cha kujengeana uwezo kati ya Taasisi hizo mbili.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Oktoba 7, 2025 lilipokea ugeni wa Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) na kufanya kikao cha kujengeana uwezo ikiwa ni mwendelezo wa juhudi za kuimarisha ushirikiano katika kusimamia na kuhifadhi mazingira nchini.

"Tumejikita katika kujadiliana mikakati, kutoa ushauri na kufanya tathmini ya utekelezaji wa shughuli za mazingira kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Taasisi hizo na kuongeza tija katika sekta ya mazingira."

*Alisema Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi, akifafanua lengo la kikao hicho*



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi (kushoto) akizungumza katika kikao cha kujengeana uwezo alipotembelewa na Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA).*

Viongozi hao pia wamejadili utekelezaji wa taratibu walizojiwekea katika kufuatilia na kusimamia Sheria za mazingira ili kuhakikisha rasilimali asilia zinatunzwa ipasavyo kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa ZEMA, Bw. Sheha Mjaja Juma alisisitiza umuhimu wa wananchi kutimiza wajibu wao kwa kufuata Sheria na taratibu za mazingira, sambamba na Taasisi za maendeleo kuhakikisha miradi yao inazingatia usimamizi endelevu wa mazingira ili kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Itakumbukwa kuwa NEMC na ZEMA wamekuwa na mashirikiano ya muda mrefu na mara kadhaa wamekuwa wakitembeleana na kupeana uzoefu kwa maslahi mapana ya Mazingira nchini Tanzania.

# ELIMU YA MAZINGIRA YATOLEWA KWA WANAFUNZI, WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA




Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa Mafunzo ya Utunzaji wa Mazingira kwa Wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Magoza iliyopo Tabata Segerea kama sehemu ya Kazimradi (Project) katika Somo la jiografia.

Mafunzo hayo yalifanyika Oktoba 7, 2025 katika Ofisi za NEMC Jijini Dar es Salaam.

*Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Magoza iliyopo Tabata Segerea wakiwa katika picha ya pamoja na maafisa Mazingira wa NEMC mara baada ya kupatiwa Elimu ya Mazingira katika Ofisi za NEMC Mikocheni jijini Dar es Salaam ikiwa ni maadhimisho ya Wiki ya Huduma kwa Mteja. Aliyesimama katikati ni Afisa Mazingira Mwandamizi Bw. Paul Kalokola, kushoto ni Mhandisi Ujenzi Bi. Beatitude Sizya na kulia ni Afisa Mazingira Bi. Florida Kavuli.*

# NEMC KANDA YA KATI YATOA MAFUNZO KWA WAKANDARASI WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA

Katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Wateja, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Ofisi ya Kanda ya Kati, Oktoba 10, 2025, lilitoa mafunzo kwa wakandarasi wa ujenzi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Mafunzo hayo yaliyofanyika katika Ofisi za Makao Makuu ya CRB, jengo la Mkandarasi House jijini Dodoma, yalilenga kuwaongezea wakandarasi uelewa kuhusu taratibu za Usimamizi wa Mazingira na umuhimu wa kutumia mifumo endelevu katika miradi ya ujenzi, ikiwemo udhibiti wa taka ngumu, taka maji na taka hatarishi.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Kaimu Meneja wa NEMC Kanda ya Kati, Bw. Novatus Mushi, alisisitiza umuhimu wa wakandarasi kuzingatia Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na kufuata viwango vya ujenzi vinavyokidhi changamoto za kimazingira, hususan mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kuathiri miundombinu.



*Kaimu Meneja wa NEMC Kanda ya Kati Bw. Novatus Mushi akitoa mafunzo kwa wakandarasi wa ujenzi waliosajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) yaliyofanyika katika jengo la Mkandarasi House jijini Dodoma.*

# NEMC NA ZEMA ZAKUBALIANA KATIKA USIMAMIZI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA NCHINI



*Watumishi wa NEMC na ZEMA wakifurahia jambo wakati wa kikao kilicholenga kuimarisha ushirikiano wa Uhifadhi na Usimamizi wa mazingira kati ya taasisi hizo mbili.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) waimarisha ushirikiano na kuingia makubaliano ya pamoja ya Uhifadhi na Usimamizi wa mazingira nchini.

Makubaliano hayo yalifikiwa katika kikao cha siku mbili kilichofanyika kuanzia tarehe 7 hadi 8 Oktoba 2025, ambapo wajumbe wa Bodi na wataalamu kutoka taasisi zote mbili walikutana kujadiliana na kubadilishana uzoefu kuhusu utekelezaji wa majukumu yao.

Kupitia kikao hicho, taasisi hizo ziliweka msingi wa ushirikiano madhubuti katika maeneo mbalimbali, yakiwemo matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika usimamizi wa mazingira, ufuatiliaji wa utekelezaji wa sheria na Kanuni za mazingira, pamoja na kuimarisha mawasiliano ya mara kwa mara kati ya pande hizo mbili.

Aidha walikubaliana pia kuhakikisha kuwa miradi yote inayotekelezwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar inazingatia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (EIA).

Akizungumza na vyombo vya habari, Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Mhandisi Mwanasha Tumbo, alisema ushirikiano huo ni hatua muhimu kuelekea utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2020/2050, ambayo inaweka mazingira kama mojawapo ya nguzo kuu za maendeleo ya Taifa.

Alisisitiza kuwa mashirikiano hayo yataongeza ufanisi katika utendaji kazi na kusaidia kufanikisha malengo ya kitaifa ya uhifadhi wa mazingira kwa maslahi ya wananchi na vizazi vijavyo.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya ZEMA, Bi. Asha Ali Khatib, alisema kikao hicho kimetoa fursa kwa wataalamu wa pande zote mbili kujifunza kutoka kwa wenzao, na pia kuibua mbinu mpya za kuboresha utendaji.

Aliongeza kuwa ushirikiano huu utawezesha uwiano wa kisera na kiutekelezaji katika masuala ya mazingira baina ya Tanzania Bara na Zanzibar.



*Picha ya pamoja ya Menejimenti ya NEMC na ZEMA mara baada ya Kikao hicho. Wa nne kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Mhandisi Mwanasha Tumbo, kulia kwake ni Mwenyekiti wa Bodi ya ZEMA Bi. Asha Ali Khatib, wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi na wa kwanza kulia ni Mkurugenzi wa ZEMA Sheha Mjaja Juma.*

# NEMC YASHIRIKI KONGAMANO JUU YA UHIFADHI WA BAHARI YA HINDI

Timu ya wataalam wa Sayansi ya bahari kutoka Tanzania ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi ambaye ni mratibu wa WIOMSA walishiriki kongamano la wadau wa masuala ya bahari lililohusisha Watunga sera, wanasayansi ya bahari, wanasheria, wahandisi wa Mazingira, wanauchumi, wafanyabiashara, watafiti, wanavyuo, wazawa na wanajamii ya Pwani ambao ni wanachama wa Jumuiya ya Wanasayansi ya bahari magharibi mwa Bahari ya Hindi kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika masuala ya Uhifadhi wa bahari ya Hindi.

Kongamano hilo la kumi na tatu (13 WIOMSA Scientific Symposium) lilifanyika kuanzia tarehe 27 Septemba hadi 3 Oktoba 2025 Mombasa nchini Kenya.

Ushiriki wa Baraza kwenye kongamano hilo kulisaidia kuongeza uelewa au kukuza taaluma ya Sayansi ya Bahari kwa wataalam wa bahari katika nyanja za Uhifadhi wa Mazingira, kupata



*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi (wa pili kulia) akiwa na Mkurugenzi Mkuu wa WIOMSA Dkt. Arthur Tude (kushoto) na baadhi ya washiriki wa Kongamano hilo.*

fursa za kukutana na wadau wanaotoa fedha za kusaidia miradi au tafiti za Mazingira ya Bahari na Bioanuai zake pamoja na kupata taasisi na mashirika mbalimbali ya kushirikiana katika tafiti na miradi ya Uhifadhi wa Mazingira ya Bahari.

Aidha ushiriki huo pia ulisaidia kuanzisha na kuimarisha mashirikiano kati ya Maafisa/ Wanasayansi ya Bahari katika nchi za Ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi, kutambua fursa za uwekezaji katika tafiti, teknolojia, biashara na uwekezaji katika sekta ya Uchumi wa Buluu pamoja na kuimarisha mahusiano ya kidiplomasia kati ya nchi wanachama wa WIOMSA.



*Timu ya NEMC ikiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi wakiwa katika picha ya pamoja na washiriki wengine wa Kongamano la WIOMSA lililofanyika Mombasa nchini Kenya.*

# NEMC KANDA YA BAGAMOYO YATOA ELIMU YA MAZINGIRA SHULE YA MSINGI NIA NJEMA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia ofisi yake ya Kanda ya Bagamoyo, ilitoa elimu ya mazingira kwa Shule ya Msingi Nia Njema, tarehe 9 Oktoba 2025.



*Meneja wa Kanda ya Bagamoyo Bi. Ndimbumi Joram akitoa Elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Nia Njema iliyopo katika wilaya ya Bagamoyo.*

Elimu hiyo iliyotolewa kwa walimu na wanafunzi ililenga kuongeza uelewa kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Katika mafunzo hayo, Meneja wa Kanda ya Bagamoyo, Bi. Ndimbumi Joram, aliwahimiza wanafunzi kuwa mabalozi wa mazingira bora kwa kuhakikisha usafi wa mazingira ya shule na majumbani mwao. Alisisitiza kuwa jukumu la kulinda mazingira sio la serikali pekee, bali ni wajibu wa kila mmoja, hasa watoto ambao ni viongozi wa kesho.

Aidha, Bi. Ndimbumi alizungumzia athari za utupaji hovyo wa taka ngumu na matumizi ya mifuko ya plastiki, akieleza kuwa plastiki ni moja ya changamoto kubwa inayoathiri mazingira duniani.

Alihimiza matumizi ya mifuko mbadala inayoweza kutumika mara nyingi kama njia mojawapo ya kupunguza taka za plastiki na kulinda afya ya mazingira.

Kwa kutambua juhudi za wanafunzi na walimu katika kushiriki kikamilifu mafunzo hayo, Meneja huyo alitoa zawadi za mifuko mbadala kama motisha na mfano wa vitendo vya ulinzi wa mazingira.

Shule ya Msingi Nia Njema iliahidi kuendeleza elimu hiyo kwa vitendo kwa kuanzisha klabu ya mazingira itakayosaidia kutunza mazingira ya shule na jamii kwa ujumla.



*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Nia Njema Pamoja na baadhi ya walimu wa shule hiyo wakifuatilia elimu ya mazingira iliyotolewa na Meneja wa Kanda ya Bagamoyo (NEMC) Bi. Ndimbumi Joram.*

# NEMC YAWAFIKIA MAAFISA WA FORODHA MIPAKANI - ELIMU YA MAZINGIRA



*Afisa Mazingira Mkuu (NEMC) Bw. Fredrick Mulinda akitoa Elimu ya Usimamizi wa Bidhaa Hatarishi zinazovuka Mipakani kupitia Mradi wa kujenga uelewa katika usimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira (EMA) katika mpaka wa Mutukula.*

> "Ni wajibu wa maafisa wote wanaohusika na usimamizi wa mipaka kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia au kutoka nchini hazina athari hasi kwa mazingira. Utekelezaji sahihi wa Sheria na Kanuni za mazingira zitasaidia kulinda afya za wananchi na kudhibiti taka hatarishi zinazoweza kuathiri mfumo wa ikolojia,"
>
> alisema Bw. Kalokola.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kupitia Mradi wa kujenga uwezo katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira (EMA), lilianza kutoa mafunzo kwa maafisa forodha waliopo mipakani, taasisi, wizara, idara pamoja na vyombo vya serikali kuhusu usimamizi wa bidhaa hatarishi kwa mazingira zinazopita mipakani.

Mafunzo hayo yalizinduliwa Oktoba 15, 2025 katika ofisi za Forodha Mtukula na yalitarajiwa kufanyika katika mipaka ya Rusumo, Kigoma na Tunduma kwa lengo la kuimarisha uelewa na uwezo wa watendaji wa serikali katika kusimamia utekelezaji wa Sheria na taratibu za mazingira kwa bidhaa zinazoingia na kutoka nchini.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Mratibu wa Mradi huo, Bw. Paul Kalokola ambaye pia ni Afisa Mazingira Mkuu wa NEMC, aliwataka washiriki kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Sheria za mazingira na kuhakikisha bidhaa zote zinazovuka mipaka zinakidhi matakwa ya kisheria.

Kwa upande wake, Kaimu Afisa Mfawidhi wa Forodha wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) – Mtukula, Bw. Elpidius Bigilwamungu, aliishukuru NEMC kwa kutoa mafunzo hayo muhimu, huku akisisitiza kuwa elimu hiyo itasaidia kuongeza ufanisi katika utambuzi na udhibiti wa bidhaa hatarishi mipakani.

Katika mafunzo hayo, wataalamu kutoka NEMC waliwasilisha mada mbalimbali zikiwemo Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Kudhibiti Taka Hatarishi, Mikataba na Miongozo ya Kimataifa ya Usimamizi wa Mazingira, na Matumizi Salama ya Zebaki.

Mafunzo haya ni sehemu ya juhudi endelevu za Serikali kupitia NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) katika kuhakikisha utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA) unafanyika kwa weledi, ushirikiano na uwajibikaji, hasa katika maeneo ya mipakani ambayo ni lango kuu la bidhaa kuingia nchini.

# NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA KIMATAIFA WA TAKA ZA KIELEKTRONIKI NCHINI KENYA



*Meneja wa Utekelezaji wa Sheria (NEMC) Bi. Amina Kibola akiwasilisha mada katika Mkutano huo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Kurugenzi ya Utekelezaji na Uzingatiaji wa Sheria lilishiriki Mkutano wa tano wa Kimataifa unaohusu masuala ya taka za kielektroniki uliofanyika kuanzia tarehe 16 na 17 Oktoba, 2025 Mombasa, nchini Kenya.

Mkutano huo umewaleta pamoja wadau kutoka Serikalini, wadau wa Maendeleo, wataalamu, Sekta binafsi pamoja na asasi za kiraia ili kujadili kwa pamoja masuala yanahusu taka za kielektroniki.

Katika mkutano huo NEMC ilishiriki katika kutoa neno la ukaribisho pamoja na kusisitiza wadau kutumia jukwaa hilo la majadiliano vizuri ili kutatua changamoto na kuibua fursa ambazo zitaleta tija katika kuhifadhi mazingira, kuongeza ajira na kukuza uchumi rejeshi.

Lengo mahususi la mkutano huo ni kuoanisha Sera, Sheria na mifumo ya Usimamizi wa taka hizo. Kujadili ukuaji wa teknolojia unaoenda sambamba na ongezeko kubwa la uzalishaji wa taka za kielektroniki.

Aidha, Uwekezaji, fursa na mbinu mbalimbali za uchakataji wa taka hizo pia ni eneo lililojadili na wadau. Mkutano pia uliangazia mitazamo mipya ya nchi za Afrika na jinsi ya kushughulikia changamoto zinazosababishwa na ongezeko kubwa la taka za kielektroniki, huku ikibainisha fursa za kuendeleza ubunifu, kuimarisha utawala, na kukuza ushirikiano wa kimataifa katika juhudi za kusimamia taka za kielectroniki kwa njia endelevu.




*Pichani ni washiriki wa mkutano wa tano wa Kimataifa unaohusu masuala ya Taka za Kielektroniki uliofayika Mombasa nchini Kenya.*

# NEMC YASHIRIKI KIKAO CHA TEKNOLOJIA ZA UREJESHAJI MAZINGIRA NCHINI AUSTRIA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki kikao cha kutathmini ya mapungufu na changamoto za teknolojia za kimazingira zinazotumika kwenye kurejesha mazingira yaliyoharibiwa au kuchafuliwa (remediation technologies).

Kikao hicho kilifanyika makao makuu ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Nishati ya Nyuklia (IAEA) yaliyopo jijini Vienna, Austria kuanzia tarehe 13-17 Oktoba, 2025.

Lengo la kikao ni kukutanisha wawakilishi kutoka nchi mbalimbali wanaohusika na Udhibiti na Tafiti katika Sekta ya Nishati ya nyuklia ili kujadili njia bora za urejeshaji wa mazingira yaliyoharibiwa au kuchafuliwa.

Njia mbalimbali za urejeshaji wa mazingira zilijadiliwa na nchi wanachama pamoja na mapungufu na changamoto zake na kujifunza njia bora inayoweza kutekelezwa na nchi husika



*Afisa Mazingira Mwandamizi (NEMC) Bi. Kuruthumu Shushu (wa pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa kikao hicho kilichofanyika jijini Vienna nchini Austria kuanzia tarehe 13-17 Oktoba, 2025.*

# NEMC NA EU YAJADILI MASUALA YA KIMAZINGIRA SEKTA YA MADINI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilikutana na muwakilishi wa ujumbe wa Umoja wa nchi za Ulaya (EU) nchini Tanzania na kujadili namna Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii zinavyofanyika kwa Tanzania na jinsi wanavyoweza kushirikiana na Baraza hususani katika masuala ya kimazingira kwa upande wa Sekta ya madini hasa madini muhimu (Critical Minerals)

Kikao hicho kilijadili miongozo iliyopo na kuainisha maeneo yanayohitaji usaidizi wao ili kuwezesha uzingatiaji wa Sheria kwa miradi ya madini inayowekezwa nchini.




*Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii Bi. Lilian Lukambuzi (wa pili kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na muwakilishi wa ujumbe wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania ambaye ni Meneja wa Programu (Utawala wa kiuchumi) Bw. Sebastian Schaber mara baada ya kujadili namna wanavyoweza kushirikiana katika masuala ya kimazingira hususani kwa upande wa Sekta ya madini hasa madini muhimu (Critical Minerals). Wa kwanza kushoto ni Kaimu Meneja wa Mapitio ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Mha. Luhuvilo Mwamila. Wa kwanza kulia ni Meneja Usajili wa Wataalam elekezi wa Mazingira (NEMC) Bi. Edika Masisi.*

# NEMC YAWANOA MAAFISA FORODHA KIGOMA - ELIMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilitoa mafunzo kwa Maafisa Forodha katika kituo cha mpakani cha Kigoma, ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa programu ya kujenga uelewa kuhusu usimamizi wa bidhaa hatarishi kwa mazingira zinazovuka mipaka.

Akifungua mafunzo hayo Oktoba 20, 2025 katika ofisi za Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Meneja wa Bandari Kigoma Bw. Edward Mabula alisisitiza umuhimu wa ushirikiano wa taasisi mbalimbali katika kulinda mazingira na kudhibiti uingizwaji wa bidhaa zisizo rafiki kwa mazingira.

Kwa upande wa wawakilishi kutoka NEMC, walieleza kuwa mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191.

Aidha, walifafanua kuwa lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Maafisa Forodha ili waweze kutambua mapema bidhaa hatarishi na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa Sheria.

Mafunzo hayo ni mwendelezo wa programu inayoendeshwa na NEMC katika vituo vya mipakani vya Mutukula, Rusumo, Kigoma na Tunduma, ikilenga kuhakikisha bidhaa zote zinazoingia au kutoka nchini zinakidhi matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.

> **"Ushirikiano baina ya taasisi kama NEMC, TRA, TPA, TBS, TMDA na wadau wengine ni muhimu sana katika kuhakikisha bidhaa zinazoingia nchini haziwezi kuathiri mazingira yetu,"**
>
> amesema Bw. Mabula.



*Wataalamu wa Mazingira kutoka NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja na Maafisa Forodha katika kituo cha mpakani cha Kigoma baada ya Mafunzo ya kujenga Uelewa kuhusu Usimamizi wa bidhaa hatarishi kwa Mazingira zinazovuka mipaka.*

# NEMC NA IUCN KUKABILIANA NA TATIZO LA UCHAFUZI WA TAKA ZA PLASTIKI UKANDA WA BAHARI



*Washiriki wa Kikao kazi cha kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa taka za plastiki katika Ukanda wa bahari.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) lilifanya kikao kazi kujadili namna bora ya kukabiliana na tatizo la uchafuzi unaotokana na taka za plastiki katika ukanda wa bahari.

Kikao hicho kimekusudia kuweka mikakati endelevu ya kudhibiti matumizi na utupaji holela wa plastiki, pamoja na kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira ya baharini kwa manufaa ya viumbe vya majini na ustawi wa binadamu kwa ujumla.

# MABADILIKO YA MATUMIZI YA ARDHI NA ATHARI ZAKE KWA UBORA WA MAJI KATIKA SEHEMU YA CHINI YA MTO MARA, TANZANIA

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi (kushoto) alipokea kitabu cha tafiti kiitwacho “Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi na Athari Zake kwa Ubora wa Maji katika Sehemu ya Chini ya Mto Mara, Tanzania” kilichoandikwa na Bi. Irene Kimario (MSc.) kama sehemu ya Shahada ya Uzamili katika Haidrojiolojia na Usimamizi wa Rasilimali za Maji.

Baraza linampongeza Bi. Irene Kimario kwa juhudi, weledi na mchango wake katika tafiti zinazochangia uelewa na usimamizi endelevu wa rasilimali za maji nchini.



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi (kushoto) akipokea kitabu cha "Mabadiliko ya Matumizi ya Ardhi na Athari Zake kwa ubora wa maji katika sehemu ya chini ya Mto Mara, Tanzania" kilichoandikwa na Bi. Irene Kimario (MSc.) (kulia).*

# NEMC YAHITIMISHA MAFUNZO KWA MAAFISA FORODHA – ELIMU YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA TUNDUMA




*Wataalamu wa Mazingira kutoka NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja na Maafisa Forodha katika kituo cha mpakani cha Tunduma baada ya kuhitimisha Mafunzo ya kujenga Uelewa kuhusu Usimamizi wa bidhaa hatarishi kwa Mazingira zinazovuka mipaka.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilihitimisha mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu usimamizi wa bidhaa hatarishi kwa mazingira zinazovuka mipaka kwa Maafisa Forodha katika kituo cha mpakani cha Tunduma, Oktoba 22, 2025. Mafunzo hayo, yaliyofanyika katika Ofisi za One Stop Border Post (OSBP) Tunduma, yalikuwa ni sehemu ya mfululizo wa mafunzo yaliyotolewa katika vituo vya Mutukula, Rusumo, Kigoma na Tunduma.

Akihitimisha mafunzo hayo Kaimu Meneja wa Forodha Tunduma, Bw. Nsajigwa Mwambegele alisisitiza umuhimu wa taasisi zote zinazohusika mipakani kushirikiana kwa karibu ili kuhakikisha bidhaa hatarishi hazivuki mipaka bila udhibiti.

“Ni wajibu wa kila taasisi kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari zitokanazo na bidhaa hatarishi. Kupitia mafunzo haya, kila mmoja ana wajibu wa kusimamia majukumu yake ili kubaini njia za panya na mbinu zote zinazotumika kuingiza bidhaa hatarishi nchini,” amesisitiza Bw. Mwambegele.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mratibu wa Mradi wa Kujenga Uwezo katika Usimamizi wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira (EMA) ambaye pia ni Afisa Mazingira Mkuu NEMC, Bw. Paul Kalokola, alisema mafunzo hayo ni sehemu ya jitihada za Serikali kupitia NEMC kuhakikisha wadau wote walioko mipakani wanakuwa na uelewa wa pamoja kuhusu namna bora ya kushughulikia bidhaa hatarishi.

Aidha, Maafisa Forodha wa kituo cha Tunduma waliishukuru NEMC kwa kutoa elimu hiyo muhimu, wakieleza kuwa imewaongezea uelewa kuhusu wajibu wao katika kulinda mazingira.

Mafunzo hayo ni sehemu ya mpango wa Baraza wa kutoa elimu endelevu kwa Maafisa Forodha katika mipaka mbalimbali ya Tanzania, hatua ambayo ni muhimu katika kuimarisha udhibiti wa bidhaa hatarishi na kuhakikisha ulinzi wa mazingira kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

# KAMISHNA TUME YA UTUMISHI WA UMMA AIPONGEZA NEMC KWA UADILIFU KATIKA UTUMISHI WA UMMA



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma, Dkt. Laurean Ndumbaro (wapili kulia) akizungumza na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi (Katikati) na baadhi ya menejimenti ya NEMC mara baada ya kikao na watumishi wa NEMC ikiwa ni ziara yake ya kikazi.*

Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma Dkt. Laurean Ndumbaro alilipongeza Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kwa kuendelea kuonesha uadilifu na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuhifadhi mazingira nchini.

Akizungumza Oktoba 23, 2025 jijini Dar es Salaam katika ziara yake ya kikazi ofisi za Baraza Dkt. Laurean Ndumbaro alisema uadilifu uliooneshwa na Baraza hilo ni mfano wa kuigwa na Taasisi nyingine za Umma katika kuhakikisha huduma kwa wananchi zinatolewa kwa ufanisi na kwa kuzingatia maadili ya kazi.

Alisisitiza kuwa uadilifu ndio nguzo kuu ya utumishi wa umma na ndio msingi wa kuaminika kwa Serikali mbele ya wananchi.

Aliongeza kuwa mafanikio ya NEMC katika utekelezaji wa miradi ya kimazingira pamoja na usimamizi wa Sheria na Kanuni za Mazingira ni ushahidi kwamba viongozi na watumishi wake wameweka maslahi ya Taifa mbele kuliko maslahi binafsi.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi alimshukuru Kamishna kwa Tathmini hiyo na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa weledi, uadilifu na ubunifu zaidi kwani pongezi hizo ni chachu ya kuongeza ari ya watumishi kulinda rasilimali za Taifa na kuhakikisha maendeleo endelevu kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Katika ziara yake Kamishna Dkt. Ndumbaro aliambatana na wataalamu wengine akiwemo Mkurugenzi wa Miongozo, Uwezeshaji na Utafiti kutoka Tume ya Utumishi wa Umma Ndugu Peleleja Masesa.



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Umma, Dkt. Laurean Ndumbaro akizungumza na Watumishi wa NEMC katika ziara yake ya kikazi, alipotembelea Ofisi za Baraza Mikocheni Jijini Dar es Salaam.*

# NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA UTEKELEZAJI WA MKATABA WA BIOANUAI, PANAMA 2025




*Mkurugenzi wa Tafiti za Mazingira (NEMC) Dkt. Menan Jangu (wa kwanza kulia mstari wa nyuma) na kulia kwake ni Meneja wa Kanda ya Bagamoyo (NEMC) Bi. Ndimbumi Joram katika picha ya Pamoja na baadhi ya washiriki wa Mkutano wa Utekelezaji wa Mkataba wa Bioanuai uliofanyika Jijini Panama.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliungana na ujumbe wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika Mkutano wa Utekelezaji wa Mkataba wa Bioanuai uliofanyika Jijini Panama kuanzia tarehe Oktoba 20 na kuhitimishwa Oktoba 30, 2025.

Tanzania, ikiwa ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Bioanuai (Convention on Biological Diversity – CBD), ilionesha dhamira yake ya kulinda na kusimamia matumizi endelevu ya bioanuai. Mkutano huu uliofanyika katika Ukumbi wa Atlapa Convention Center na ulihusisha mikutano miwili mikubwa: SABSTTA-27, iliyojadili masuala ya kisayansi, kiufundi na kiteknolojia kuhusu bioanuai; na SB8J-1, inayohusiana na haki na mchango wa jamii za wenyeji katika hifadhi ya bioanuai.

Kupitia ushiriki wake, NEMC iliungana na wadau mbalimbali wakiwemo Ofisi ya Makamu wa Rais, taasisi za Wizara ya Maliasili na Utalii (TFS na TAWA), pamoja na Shirika la The Nature Conservancy (TNC). Majadiliano katika mikutano hii yalijikita kwenye utekelezaji wa Mkakati wa Dunia wa Kuhifadhi Bioanuai (Kunming–Montreal Global Biodiversity Framework – KMGBF) uliopitishwa mwaka 2022, yakilenga kuweka miongozo ya kuboresha sera, sheria na programu za kitaifa kuhusu hifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za asili.

Aidha, mada kuu zinazojadiliwa ni pamoja na bioanuai na mabadiliko ya tabianchi, bioanuai na afya, viumbe vamizi, bioanuai na kilimo, pamoja na tathmini za athari za viumbe hai vilivyobadilishwa kijenetiki (LMOs).

Kwa Tanzania, ushiriki huo ni fursa muhimu ya kubadilishana uzoefu na mataifa mengine kuhusu njia bora za kudhibiti upotevu wa bioanuai na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kupitia jukwaa hilo, NEMC iliimarisha nafasi yake katika kuunganisha taaluma, sayansi, na jamii katika utekelezaji wa KMGBF, sambamba na kuandaa mapendekezo yatakayowezesha utekelezaji bora wa sera za mazingira nchini.

Vilevile, majadiliano hayo yalitoa nafasi ya kuandaa msimamo wa pamoja wa kikanda kuelekea Mkutano wa 17 wa Mkataba wa Bioanuai utakaofanyika Jijini Yerevan, Armenia mwaka 2026.

Kwa ujumla, ushiriki wa NEMC katika mkutano huo ni ushahidi wa dhamira ya Tanzania katika kulinda mazingira na kuhimiza matumizi endelevu ya rasilimali za asili. Ulisisitiza kuwa uhifadhi wa bioanuai ni nyenzo muhimu katika kulinda afya ya jamii, kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, na kuhakikisha usalama wa chakula.

NEMC inaendelea kushirikiana na wadau wa ndani na wa kimataifa kuhakikisha malengo ya kimataifa ya bioanuai yanatekelezwa kwa ufanisi kwa manufaa ya taifa na dunia kwa ujumla.

# NEMC YAJINASIBU KUFANYA MAKUBWA SHIMMUTA 2025, YAPOKEA VIFAA KUTOKA MRADI WA ADAPTATION FUND

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilijipanga kisawasawa kushiriki mashindano ya michezo yaliyoratibiwa na Shirikisho la Michezo la Mashirika ya Umma, Taasisi na Makampuni binafsi Tanzania (SHIMMUTA) ambapo tarehe 28 Oktoba, 2025 lilizindua rasmi vifaa vilivyofadhiliwa na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation fund) vitakavyotumika na wanamichezo katika mashindano hayo.

Akizungumza wakati kukabidhi vifaa hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi alisema michezo ni muhimu kwa Afya ya binadamu kwani hupelekea uwezo wa kufanya kazi vizuri huku akisisitiza usimamizi na uhifadhi wa Mazingira nchini

Aliongeza kuwa ushiriki wa NEMC katika michezo hiyo ni fursa muhimu ya kuifikia jamii, kuimarisha ushirikiano baina ya watumishi wa Umma na Sekta binafsi.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Michezo - NEMC Bw. Fortinatus Patrick alisema timu za NEMC ziko tayari kwenda kupambana katika michezo yote na wamejiandaa kufanya vizuri katika mashindano ya mwaka huu.

Naye Mkurugenzi wa Utawala na Fedha (NEMC) Bw. Dickson Mjinja ambaye ni mlezi wa timu hiyo, alipozungumza alisema NEMC ilijipanga kisawasawa kuwa washindani na si washiriki katika michezo yote iliyojisajili.

NEMC kwa kushirikiana na Mradi wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi ilifanikisha Mandalizi hayo ya SHIMMUTA 2025 yaliyotarajiwa kufanyika jijini Mwanza November 13 - 29, 2025 huku yakilenga kuelimisha umma wa watanzania kuhusu mazingira na masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi.



*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Dkt. Immaculate Sware Semesi (wapili kushoto) akimkabidhi Jezi Afisa Mazingira Mkuu Bw. Fredrick Mulinda katika uzinduzi wa vifaa vya michezo vitakavyotumika katika mashindano ya michezo ya SHIMMUTA-2025 vilivyofadhiliwa na Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund)*



*Hafla ya uzinduzi wa vifaa vya mashindano ya michezo ya SHIMMUTA 2025*

# NEMC KANDA YA MAGHARIBI YAPATA MAFUNZO YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA




*'Wataalam wa Mazingira na watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Magharibi wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kupata mafunzo ya Tathimini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) Mstari wa nyuma, wa katikati ni Meneja wa Kanda hiyo Bw. Edgar Mgila. Kushoto ni Kaimu Meneja wa Mapitio ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Mha. Luhuvilo Mwamila, kulia ni Meneja Usajili wa Wataalam elekezi wa Mazingira (NEMC) Bi. Edika Masisi.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Kurugenzi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii ilitoa mafunzo ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira kwa wataalamu elekezi wa mazingira na watumishi wa Baraza waliopo Kanda ya Magharibi inayohusisha mikoa mitatu (Kigoma, Katavi na Tabora) kuanzia tarehe 1-3 Oktoba, 2025.

Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuboresha ufanyaji wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) na upitiaji wa taarifa za TAM zilizowasilishwa Baraza.

# NEMC YAADHIMISHA WIKI YA HUDUMA KWA WATEJA KWA VITENDO

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) katika kuadhimisha Wiki ya Huduma kwa Mteja yenye kaulimbiu "***Mission Possible***" liliweka banda maalum katika ofisi zake ili kurahisisha huduma kwa wateja wake.

Banda hilo lililenga kuboresha mawasiliano na kujenga mahusiano bora yenye kutoa fursa kwa wadau kutoa maoni, changamoto, pamoja na kupatiwa majibu ya papo kwa papo kuhusu huduma za mazingira.

Katika hatua nyingine Baraza Kupitia Kanda zake 13 liliendelea kutoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kufanya ziara za ukaguzi (site visits) kwa wadau wake kujiridhisha na utekelezaji wa Kanuni za mazingira na kushughulikia changamoto zilizoibuliwa na wananchi.




*Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi (kushoto) akiwa katika banda maalum la kuhudumia wateja lililowekwa Ofisi za NEMC katika msimu wa Wiki ya Huduma kwa Mteja iliyoadhimishwa kuanzia tarehe 6 hadi 10 Oktoba, 2025.*

# NEMC YASHIRIKI KIKAO KAZI KUHUSU AKILI MNEMBA NA MASOKO YA KIDIGITALI

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki kikao kazi kilichoratibiwa na Chama Cha maafisa Habari wa Serikali (TAGCO) kuhusu matumizi ya akili mnemba na Masoko kidigitali katika kufanya Mawasiliano Serikalini (Artificial intelligence (AI) and Digital Marketing in Government) kilichofanyika Jijini Arusha.



*Kaimu Meneja wa kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa umma (NEMC) (wa kwanza kushoto) na Afisa Mawasiliano na uhusiano kwa umma (NEMC) Bi. Aziza Muhali wakishiriki kikaokazi kilichoratibiwa na Chama cha Maafisa Habari wa Serikali (TAGCO) kuhusu matumizi ya akili mnemba na Masoko kidigitali katika kufanya Mawasiliano Serikalini (Artificial intelligence (AI) and Digital Marketing in Government Communication kilichofanyika Jijini Arusha.*

Kikao hicho kililenga kuwawezesha maafisa habari hao namna sahihi ya matumizi ya akili mnemba yaliyolenga kurahisisha utekelezaji wa majukumu na kuongeza ujuzi na ufanisi katika Utekelezaji wa majukumu.

Mada zilizofundishwa ni pamoja na matumizi ya akili mnemba katika Mawasiliano ya kimkakati, akili mnemba katika Mawasiliano na masoko, akili mnemba katika kupata maoni na mrejesho kutoka kwenye jamii na Mawasiliano na masoko wakati wa maafa (Crisis communication).

Kikao Kazi hicho kilifanyika jijini Arusha kuanzia Novemba 10-14, 2025 ambapo NEMC iliwakilishwa na Kaimu Meneja wa Uhusiano na Ma wasiliano, Bi. Martha Kawishe na Afisa Uhusiano na Mwasiliano, Bi. Aziza Muhali.



*Washiriki wa kikao kazi kikaokazi kilichoratibiwa na Chama cha Maafisa Habari wa Serikali (TAGCO) wakifuatilia kikao hicho kilichohusu matumizi ya akili mnemba na Masoko kidigitali katika kufanya Mawasiliano Serikalini (Artificial intelligence (AI) and Digital Marketing in Government Communication kinachofanyika Jijini Arusha.*

# NEMC YAENDESHA MAFUNZO YA NDANI JUU YA MCHAKATO WA KUPITIA MIRADI YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA



*Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Bi. Lilian Lukambuzi akizungumza katika mafunzo ya kuwajengea uwezo watumishi wa NEMC juu ya mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kaguzi za Mazingira katika Ofisi za NEMC jijini Dar es Salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliandaa mafunzo maalum ya siku nne kwa watumishi wake wa kanda za Dar-es-salaam yenye lengo la kuwajengea uwezo juu ya mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kaguzi za Mazingira ili kuwaongeza ufanisi katika mapitio ya miradi husika.

Mafunzo hayo yalifunguliwa rasmi 18 Novemba 2025 na Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Bi. Lilian Lukambuzi na kuhitimishwa Novemba 21, 2025.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mkurugenzi Bi. Lilian Lukambuzi alisisitiza umuhimu wa Sheria ya Mazingira na Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira ya 2005 na marekebisho yake (2018) na 2024 katika mchakato wa mapitio ya Miradi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira.

Aidha, alisisitiza watumishi kujikita katika mapitio thabiti ya miradi ili kuwa na mipango bora ya Usimamizi wa mazingira na Ufuatiliaji itakoyeleta uendelevu wa miradi husika.

Watoa mada katika mafunzo hayo walikuwa ni wataalamu waandamizi wa Mazingira wakiwemo Kaimu Meneja wa Mapitio ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii, Mhandisi Luhuvilo Mwamila na Meneja Usajili wa Wataalam elekezi wa Mazingira, Bi. Edika Masisi ambaye alijikita katika kuelezea kwa kina hatua za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na vigezo vya kuzingitia katika mapitio ya Miradi na namna bora ya uandaaji wa ripoti za TAM na Kaguzi za Mazingira.



*Wataalam wa Mazingira (NEMC) wakifuatilia mafunzo hayo yaliyolenga kuwajengea uwezo juu ya mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kaguzi za Mazingira ili kuwaongeza ufanisi katika mapitio ya miradi husika.*

# NEMC YASHIRIKI UNFCCC COP-30, BELEM, NCHINI BRAZIL

## Ushiriki wake kuleta manufaa kwenye miradi na mazingira

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki Mkutano wa thelathini wa nchi wanachama wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC COP-30), uliofanyika jijini Bélem, nchini Brazil kuanzia tarehe 03/11/2025 na kuhitimishwa tarehe 21/11/2025.

Akiongoza ujumbe wa NEMC katika Mkutano huo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Mhandisi Mwanasha Tumbo aliyeambatana pia na Makamu Mwenyekiti, Wakili Alex G. Mgongolwa aliwataka watumishi wa Baraza kuhakikisha wanatumia vyema jukwaa la mkutano huo kupata fursa za fedha za miradi ili kuweza kuhakikisha unaleta matokeo chanya katika kutekeleza vyema nguzo ya mazingira katika Dira ya Taifa ya 2050.

Katika kutekeleza hilo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi, aliongoza ujumbe wa NEMC kwenye Mikutano mbalimbali ya uwili ili kuimarisha ushirikiano na wadau katika sekta ya Mazingira.

Baadhi ya Mikutano hiyo ni pamoja na mkutano wa uwili na Benki ya Maendeleo ya Africa (African Development Bank), uliohusu kuanza kwa mradi uliowasilishwa na Baraza na kupitishwa na benki hiyo. Mradi huo wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 15 ulilenga kutatua changamoto za



*Uongozi wa Bodi pamoja na timu ya wataalam iliyoambatana na ujumbe wa NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja baada ya kushiriki Mkutano wa thelathini wa nchi wanachama wa Mkataba wa Kimataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (UNFCCC COP-30), uliofanyika jijini Bélem, nchini Brazil.*

mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya pwani yaani Dar es Salaam, Pwani na Pemba.

Aidha, Dkt. Semesi alikutana pia na Sekretarieti ya Mfuko wa Kimataifa wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (Adaptation Fund-AF) ambapo aliweza kuwahimiza Adaptation Fund kukamilisha taratibu za kulipatia Baraza ithibati ya pili (reaccreditation) sambamba na kukamilisha mapitio ya miradi iliyowasilishwa yenye jumla ya thamani ya Dola za Marekani milioni 35. Katika mazungumzo hayo, mfuko wa Adaptation Fund ulilihakikishia Baraza kwamba taratibu za ithibati zilitarajiwa kukamilika ndani ya wiki chache kuelekea mwishoni mwa mwaka huu.

Hata hivyo Adaptation Fund iliidhinisha ripoti za mwaka za miradi ya SWAHAT na Bunda inayosimamiwa na Baraza Pamoja na kuachilia kiasi cha takribani Dola za Marekani laki 4 ili kukamilisha utekelezaji wa miradi hiyo.

Sambamba na hayo, Dkt. Semesi aliongoza ushiriki katika vikao mbalimbali vya kitaalam, mikutano ya pembezoni pamoja na kuanzisha mchakato wa mashirikiano na taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi ili kupanua wigo wa kujipatia fedha za kupambana na mabadiliko ya tabianchi. Baadhi ya taasisi hizo ni pamoja na Mfuko wa Kitaifa wa Maji (National Water Fund), Pew Charitable Trust, Benki ya Dunia, Global Climate Mobility, Global Methen Hub, IUCN na Ocean Vision.

Timu ya wataalam iliyoambatana na ujumbe wa Bodi kwenye Mkutano huo ni pamoja na Dkt Careen Kahangwa, Bw. Fredrick Mulinda, Bw, Paul Kalokola, Bi. Jackline Nyantori na Bw. Rahim Kantinga.

# NEMC YAENDESHA MAFUNZO YA NDANI JUU YA MAPITIO YA TAARIFA ZA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NA JAMII NA KAGUZI ZA MAZINGIRA



*Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Bi. Lilian Lukambuzi akiwasilisha mada katika mafunzo hayo*



*Watumishi wa NEMC wakipata mafunzo kuhusu mapitio ya taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) pamoja na kaguzi za mazingira katika ukumbi wa baraza jijini Dar es Salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia Kurugenzi ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii liliwajengea uwezo watumishi wake kwa kuendesha mafunzo ya ndani yahusuyo mapitio ya taarifa za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (TAM) pamoja na kaguzi za mazingira.

Mafunzo hayo ya siku nne yalifanyika kuanzia tarehe 18 hadi 21 Novemba 2025 yakilenga kuongeza weledi na kuimarisha utendaji katika kupitia taarifa na kufanya kaguzi za miradi inayowasilishwa kwa Baraza, kuimarisha umahiri wa watumishi hao na kuandaa timu madhubuti yenye uwezo wa kushughulikia kwa haraka na kwa ubora wa juu taarifa za tathmini na kaguzi za mazingira zinazowasilishwa na wawekezaji kwa Baraza.

Mafunzo haya yalifunguliwa rasmi na Mkurugenzi wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii, Bi. Lilian Lukambuzi, na kuendeshwa na wataalamu kutoka ndani ya Kurugenzi hiyo wakiwemo Eng. Luhuvilo Mwamila "Kaimu Meneja Mapitio ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii" na Bi. Edika Masisi "Meneja Usajili wa Wataalamu Elekezi wa Mazingira". Washiriki walipata nafasi ya kujifunza kwa undani namna bora za kufanya mapitio ya taarifa za TAM, vigezo vya tathmini, na hatua muhimu katika ukaguzi wa mazingira ili kuhakikisha miradi inazingatia sheria ya Mazingira.

Aidha, mafunzo hayo yaliwalenga watumishi wa NEMC kutoka kanda za Mashariki Kaskazini, Mashariki Kusini, Ilala, Temeke, Bagamoyo pamoja na Makao Makuu.

# NEMC YAPATA MAFUNZO YA UTEKELEZAJI WA DIRA YA MAENDELEO YA TAIFA 2050

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliendesha mafunzo maalumu ya kujengeana uwezo kuhusu namna ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, yakiangazia kwa kina Nguzo ya Tatu inayohusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mafunzo hayo yalifanyika jijini Dar es Salaam yakiongozwa na Profesa Noah Makula akishirikiana na Mhe. Prof Pius Yanda kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na kushirikisha wajumbe wa Bodi pamoja na menejimenti ya Baraza.




*Profesa Noah Makula akiwasilisha mada katika mafunzo hayo yaliyolenga kujengeana uwezo kuhusu namna ya kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, yakiangazia kwa kina Nguzo ya Tatu inayohusu Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi.*

Katika mafunzo hayo, washiriki walipata elimu kuhusu matarajio ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050 ambayo inalenga kuifanya Tanzania kuwa taifa lenye ustahimilivu, ubunifu, ustawi na diplomasia kabla ya kufikia karne ya 21 kwa kuzingatia misingi ya demokrasia, haki, utu, amani, umoja na maadili ya kitaifa.

Aidha, katika kuadhimisha mchango wa wataalam waliolisaidia Taifa katika masuala ya mazingira, NEMC imemtunuku Profesa Pius Zebhe Yanda tuzo ya heshima kwa mchango wake mkubwa na wa muda mrefu katika kubuni na kuelekeza utekelezaji wa Nguzo ya Tatu ya Dira ya 2050. Nguzo hiyo inahusu uhifadhi wa bioanuai, ulinzi wa ardhi oevu na vyanzo vya maji, udhibiti wa uchafuzi wa mazingira, usimamizi wa ardhi pamoja na kuongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza baada ya kutolewa kwa tuzo hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi alipongeza hatua hiyo na kusisitiza dhamira ya Baraza kuhakikisha kuwa utekelezaji wa Nguzo ya Tatu unazingatiwa ipasavyo kwa mustakabali endelevu wa mazingira nchini.

Katika hatua nyingine, wajumbe wa Bodi na Menejimenti walipitia tathmini ya Mpango Mkakati wa Baraza wa miaka mitano. Wasilisho hili lilitolewa na Dkt. Joshua Mwakujonga kutoka Chuo cha Mzumbe ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya Mpango mkakati wa Baraza wa miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2026/27- 2030/31.



*Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Mhandisi Mwanasha Tumbo (kulia) na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi wakifuatilia mafunzo hayo.*



*Sehemu ya Menejimenti ya Baraza wakifuatilia mafunzo hayo*

# NEMC YAELIMISHA UMMA UDHIBITI WA KELELE CHAFUZI NA MITETEMO




*Meneja wa Uzingatiaji wa Sheria (NEMC) Bw. Hamadi Taimuru (kulia) akizungumza na vyombo vya Habari kuhusu elimu ya udhibiti wa kelele chafuzi na mitetemo.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliendelea kuimarisha juhudi za kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele na mitetemo kufuatia ongezeko la malalamiko katika maeneo ya mijini na vijijini.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam, Bw. Hamadi Taimuru, Meneja wa Uzingatiaji wa Sheria (NEMC), alisema kelele zimeendelea kuwa changamoto kubwa kwa afya na ustawi wa wananchi kutokana na shughuli za burudani, ujenzi, biashara na matumizi ya vifaa vya sauti vinavyokiuka viwango vya kisheria.

Bw. Taimuru alifafanua kuwa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (Sura 191) na Kanuni za Udhibiti wa Kelele na Mitetemo za mwaka 2015 zimeweka viwango maalumu vya kelele kwa maeneo ya makazi, biashara, viwanda na Taasisi muhimu kama Hospitali na shule, sambamba na kuainisha utaratibu wa utoaji vibali kwa shughuli zinazoweza kusababisha kelele kubwa.

Alisema athari za kelele za muda mrefu ni pamoja na kupoteza usikivu, msongo wa mawazo, shinikizo la damu na kuathiri umakini wa watoto shuleni, hivyo kulifanya suala la udhibiti kuwa muhimu kwa kulinda afya ya umma".

Aidha, alibainisha uwepo wa changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa Kanuni za udhibiti, ikiwemo uhaba wa vifaa vya kupimia kelele kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uelewa mdogo wa wananchi kuhusu athari za kelele, pamoja na baadhi ya biashara na maeneo ya burudani kutokufuata sheria na muda wa utulivu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, viwango vinavyoruhusiwa ni 70dBA mchana na 60dBA usiku kwa maeneo ya viwandani; 50dBA mchana na 35dBA usiku kwa makazi, 60dBA mchana na 50dBA usiku kwa makazi yenye viwanda vidogo, 55dBA mchana na 45dBA usiku kwa maeneo ya makazi, biashara na burudani; na 45dBA mchana na 35dBA usiku kwa Hospitali, Shule, Kumbi za mikutano na maeneo ya mapumziko.

Katika kuimarisha usimamizi, Bw. Taimuru alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya OSHA, Polisi, BASATA, Serikali za Mitaa, nyumba za ibada na wamiliki wa kumbi za burudani katika kutekeleza majukumu yao, ikiwemo kusimamia vibali, kutoa elimu, kuhakikisha matumizi sahihi ya vifaa vya sauti na kufanya kaguzi za mara kwa mara.

Aliongeza kuwa ramani za viwango vya kelele, kampeni za uelimishaji na mifumo rahisi ya utoaji taarifa za malalamiko ni hatua muhimu zinazohitajika kuimarishwa.

Akihitimisha, Bw. Hamadi Taimuru amesema Tanzania ina mfumo madhubuti wa kisheria wa kudhibiti kelele na mitetemo, na kwamba ushirikiano wa wadau wote, sekta binafsi, Taasisi za umma na wananchi ni msingi muhimu wa kulinda afya, utulivu na ustawi wa jamii.



*Baadhi ya waandishi wa Habari waliohudhuria Mkutano huo.*

# NEMC YAILAZA WCF 5 BILA SHIMMUTA 2025

Timu ya mpira wa miguu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ililaza timu ya WCF kwa jumla ya magoli matano kwa sifuri.

Mchezo huo uliochezwa Novemba 27, 2025, katika uwanja wa Highland mkoani Morogoro, ulianza kwa kasi kubwa ambapo dakika ya 15 Fortinatus Patrick alifungua ukurasa wa mabao kupitia mkwaju wa penati, na kufanya "mazingira ya uwanja" kuanza kuwa safi. Bao hilo lilidumu hadi dakika ya 33 ambapo mfungaji huyo huyo, Fortinatus Patrick, alipachika bao la pili lililoipeleka NEMC mapumzikoni wakiwa kifua mbele, huku "mazingira" yakiendelea kupendeza uwanjani.

Kipindi cha pili kilipoanza dakika ya 46, Fortinatus Patrick aliendeleza ubabe kwa kufunga bao la tatu, kabla ya kiungo Ismail Jemba kuongeza la nne dakika ya 51.

Kama ilivyo desturi ya NEMC kutoridhishwa na uchafuzi wa mazingira nchini na kuendelea kuhimiza usafi kote nchini, vivyo hivyo hawakuridhika na matokeo hayo ya 4–0. Dakika ya 62, Emmanuel Mlungwana alipiga shuti kali kutoka katikati ya uwanja lililopenya kati ya miguu ya golikipa wa WCF na kutinga wavuni, likiwa bao la tano kwa NEMC.

NEMC ilikuwepo mkoani Morogoro kushiriki michezo ya SHIMMUTA 2025 kama sehemu ya kuimarisha afya za watumishi wake pamoja na kuendelea kutoa hamasa kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini. Kwa mwaka huu, timu za NEMC zilifadhiliwa jezi na vifaa vya michezo kupitia miradi yake miwili — Adaptation Fund na EHPMP — huku zikitumia jezi hizo kueneza jumbe mbalimbali kuhusu mabadiliko ya tabianchi na udhibiti wa matumizi ya zebaki (mercury).






*Baadhi ya wachezaji wa Timu ya mpira wa miguu (NEMC) wakiwa katika picha ya Pamoja katika uwanja wa Highland mkoani Morogoro ulipochezwa mchezo huo.*



*Wachezaji wa mpira wa miguu wa timu ya NEMC na timu ya WCF wakikaguliwa na waamuzi na viongozi wa SHIMMUTA kabla ya kuanza kwa mchezo huo.*

# DKT. FESTO DUGANGE AZUNGUMZA NA WATUMISHI WA NEMC

- **Asisitiza Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira hasa udhibiti wa kelele chafuzi maeneo ya makazi.**



*Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Dkt. Festo Dugange akizungumza na Menejimenti ya NEMC alipotembelea Ofisi za NEMC ikiwa ni ziara yake ya kwanza ya kikazi tangu kuteuliwa kwake.*

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) Mhe. Dkt. Festo Dugange, alifanya ziara yake ya kwanza katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na kuzungumza na watumishi wa Baraza hilo, akitoa maelekezo mahsusi juu ya kuimarisha usimamizi wa mazingira nchini.

Katika hotuba yake, Dkt. Dugange alisisitiza umuhimu wa kulinda afya ya jamii kupitia udhibiti wa kelele chafuzi, akibainisha kuwa kelele zimekuwa chanzo cha changamoto za kiafya, hususani magonjwa yasiyoambukiza katika maeneo ya makazi.

Alisema kelele chafuzi ni miongoni mwa mambo yanayoashiria uharibifu wa mazingira na yanapaswa kudhibitiwa kwa nguvu na umakini wa hali ya juu.

Akiweka msisitizo zaidi, Dkt. Dugange ameagiza NEMC kuandaa mpango mkakati wa mashirikiano kati yake na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) hasa kwenye majiji ili kuhakikisha udhibiti wa kelele chafuzi unatekelezwa katika ngazi zote kutoka Mtaa hadi Taifa.

Alisisitiza kuwa kila mtumishi wa NEMC ana jukumu la kuhakikisha jamii inajengewa uelewa na Sheria za Mazingira zinatekelezwa ipasavyo.

Katika mazungumzo hayo, Dkt. Dugange pia aliuzungumzia Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2050 unaohusisha nguzo tatu kuu, ikiwemo Uhifadhi wa Mazingira na Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Alifafanua uhusiano uliopo kati ya mazingira salama, afya bora, na kupungua kwa magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Akigusia ajenda ya nishati safi, Dkt. Dugange alikumbusha kuwa Serikali ya Awamu ya Sita inataka ifikapo mwaka 2034, asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ambayo ina manufaa kwa jamii ikiwemo kupunguza uchafuzi wa hewa, kulinda mazingira na kupunguza gharama za maisha.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC, Mhandisi Mwanasha Tumbo, aliahidi kusimamia utekelezaji wa maelekezo yote yaliyotolewa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt.Immaculate Sware Semesi alipokea maelekezo na kuahidi kuyatekeleza kwa mujibu wa Sheria na kuhakikisha usimamizi thabiti wa mazingira nchini.

# NEMC YAENDESHA MAFUNZO KUHUSU NYENZO ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA WIZARA, TAASISI NA HALMASHAURI ZA MANISPAA NA WILAYA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) liliendesha mafunzo kuhusu nyenzo za usimamizi wa mazingira kwa Wizara, Taasisi pamoja na Halmashauri za Manispaa na Wilaya nchini. Mafunzo haya yaliandaliwa kupitia Mradi wa kujenga uwezo wa kitaifa katika kusimamia Sheria ya usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Mradi huu ulifadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA). Mradi ulilenga kuimarisha uelewa na uwezo wa watumishi katika kusimamia Sheria ya mazingira kwa ufanisi katika utekelezaji wa majukumu katika maeneo yao ya kazi.




*Meneja wa Maeneo Maalum na Mabadiliko ya Tabianchi (NEMC), Dkt. Careen Kahangwa akiwasilisha mada katika mafunzo hayo.*

Mafunzo hayo ya siku mbili yalianza tarehe 27 hadi 28 Novemba 2025 jijini Dodoma. Kupitia mafunzo hayo, washiriki walipata maarifa ya kutathmini athari za kimazingira pamoja na kupanga mikakati endelevu ya utunzaji wa mazingira huku wakizingatia Nguzo ya tatu ya Dira ya maendeleo ya Taifa 2050 ambayo iliweka mkazo juu ya kuzingatia masuala ya utunzaji wa Mazingira nchini.

Akifungua mafunzo hayo, Meneja wa maeneo maalum na mabadiliko ya tabianchi kutoka NEMC, Dkt. Careen Kahangwa, aliwataka washiriki kutumia fursa hiyo kuboresha utendaji katika maeneo yao ya kazi. Mafunzo haya yaliendeshwa na timu ya wataalamu kutoka NEMC. Aidha wataalamu kutoka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Ofisi ya Makamu wa Rais na taasisi binafsi ya Taka ni ajira nao walishiriki Katika kutoa mafunzo.



*Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya kuhusu nyenzo za usimamizi wa mazingira wakifuatilia mafunzo hayo.*

Washiriki wa mafunzo hayo walipata nafasi ya kujadili kwa kina changamoto za kimazingira zilizojitokeza katika taasisi zao na kujifunza mbinu bora za kukabiliana na changamoto hizo. Kupitia mafunzo hayo, yalitarajiwa kuboresha mifumo ya ufuatiliaji, utoaji taarifa, na utekelezaji wa sheria na kanuni za mazingira nchini. Hatua hiyo muhimu ilichangia kwa kiasi kikubwa kulinda na kuhifadhi mazingira kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

# NEMC YASAINI MAKUBALIANO YA AWALI NA UPS KUANZISHA MFUMO WA KIDIGITALI WA UFUATILIAJI WA UCHAFUZI WA MAZINGIRA




*Mkurugenzi wa Sheria (NEMC) Bw. Joannes Karungura (kulia) pamoja na Afisa Mkuu wa Mikakati na Mapato Bw. Mamadou Drame (UPS) wakisaini hati za makubaliano ya awali ya kuanzisha mfumo wa kidigitali wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira yaliyofanyika Disemba 4, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa NEMC jijini Dar es Salaam.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilisaini makubaliano ya awali na Kampuni ya United Platform Solution (UPS) kwa ajili ya kuanzisha mfumo wa kidigitali wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira katika miradi yote ya maendeleo nchini.

Hafla hiyo ya kusaini makubaliano hayo ilifanyika Disemba 04, 2025 katika ukumbi wa mikutano wa Baraza uliopo jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Bw. Dickson Mjinja ambaye pia ni Mkurugenzi wa Utawala na Fedha, alisema Baraza limefikia hatua hiyo ili kurahisisha masuala mazima ya usimamizi na uhifadhi wa mazingira kwani mfumo huo ukikamilika utarahisisha kubaini viashiria vya uchafuzi wa mazingira na kupata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu hali ya mazingira.

Naye Bw. Mamadou Drame kutoka UPS alipozungumza alisema imekuwa azma yao kushirikiana na NEMC katika kuhakikisha uchafuzi wa Mazingira unadhibitiwa kidigitali ili kuyalinda kwa maendeleo endelevu.

Akifafanua namna mfumo huo utakavyotenda kazi, Kaimu Mkurugenzi wa Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria wa NEMC, Bw. Jamal Baruti alisema kwa sasa utaanza mradi wa majaribio ambapo vifaa maalum vitawekwa katika miradi ya mazingira ikijumuisha miradi iliyopo katika Kanda 13 za NEMC nchi nzima hali itakayoimarisha zaidi usimamizi na Uhifadhi wa mazingira nchini.



*Mkurugenzi wa Utawala na Fedha Bw. Dickson Mjinja (katikati) na Afisa Mkuu wa Mikakati na Mapato Bw. Mamadou Drame (wapili kushoto) kutoka UPS wakionesha hati ya makubaliano ya awali ya kuanzisha mfumo wa kidigitali wa ufuatiliaji wa uchafuzi wa mazingira katika miradi yote ya maendeleo nchini iliyosainiwa kati ya taasisi hizo mbili Disemba 04, 2025 katika Ukumbi wa Mikutano wa NEMC jijini Dar es Salaam.*

# NEMC YAENZI MAADHIMISHO YA SIKU YA WALEMAVU DUNIANI



*Afisa Utumishi Mkuu wa NEMC, Bi. Shukrani Haule (kushoto) akitoa ujumbe kwa watoto wenye ulemavu katika kituo cha Erick Memorial mkoani Morogoro kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Immaculate Sware Semesi wakati timu ya michezo ya NEMC ilipotembelea kituo hicho Disemba 4, 2025 ikiwa ni maadhimisho ya siku ya kimataifa ya watu wenye ulemavu.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia timu yake ya wanamichezo walioshiriki mashindano ya SHIMMUTA 2025 walitembelea Kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu cha Erick Memorial Faundation kilichopo mkoani Morogoro Disemba 4, 2025.

Timu hiyo ya NEMC ilipata fursa ya kutembelea, kufariji na kuwapa misaada ya vyakula na vifaa vya usafi pamoja na kutoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ikiwa ni sehemu ya kuienzi siku maalumu ya walemavu ambapo duniani kote hufanyika tarehe 3 Disemba ya kila mwaka.

Akizungumza kwenye kituo hicho kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Afisa Utumishi Mkuu wa NEMC Bi. Shukrani Haule alisema Baraza linaendelea kushirikiana na watu wa makundi yote katika kuhakikisha Mazingira yanakuwa safi na salama kwa watu wote, lakini pia kihakikisha makundi haya yanawezeshwa na kujumuishwa katika maamuzi yanayozingatia Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini.

"Baraza katika kutekeleza majukumu yake linashirikiana na watu wote na kundi hili la watu wenye ulemavu limekuwa likilizingatiwa siku zote katika mipango yake yote" Alisema Bi. Shukrani.

Naye Mtendaji wa Taasisi hiyo ya Erick Memorial, Bw. Robert Mkalawa alitoa wito kwa Taasisi za Serikali kuona umuhimu wa siku hii kama ambayo NEMC imefanya.

"Tunashukuru kutembelewa Taasisi inayohusika na Mazingira ambao ni NEMC na hii inadhihirisha kuwa hakuna Mazingira bila watu na watu wenyewe ndio sisi bila kubagua, lakini nitoe rai kwa Taasisi nyingine za Serikali kuiga mfano wa NEMC katika kuadhikisha siku hii ya Walemavu Duniani". Alisema Bw. Robert.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Michezo NEMC Bw. Fortinatus Patrick alisema kilichofanyika ni muendelezo wa kile alichokisisitiza Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi katika kuweka Mazingira wezeshi kwa makundi yote kujumuisha jamii za watu wenye ulemavu katika kuhifadhi Mazingira nchini.




*Wanamichezo wa NEMC walioshiriki mashindano ya SHIMMUTA 2025 walipotembelea Kituo cha kulelea watoto wenye ulemavu cha Erick Memorial mkoani Morogoro, kufariji na kuwapa misaada ya vyakula na vifaa vya usafi pamoja na kutoa elimu ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ikiwa ni sehemu ya kuienzi siku maalumu ya walemavu ambapo duniani kote hufanyika tarehe 3 Disemba ya kila mwaka.*




*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mwere wakiwa na vifaa vya usafi vilivyokabidhiwa na wanamichezo wa timu ya NEMC iliyoshiriki mashindano ya michezo **SHIMMUTA 2025** ikiwa ni sehemu katika uhamasishaji wa usafi wa mazingira*

# NEMC YAHAMASISHA USAFI WA MAZINGIRA SHIMMUTA 2025 - MOROGORO

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kupitia wanamichezo wake walioshiriki mashindano ya SHIMMUTA 2025 mkoani Morogoro wakichagizwa na kauli mbiu yao isemayo "Michezo ni Afya, Mazingira ni Uhai" walishiriki zoezi la kufanya usafi kwenye uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro siku ya kufunga mashindano hayo Disemba 6, 2025.

Wanamichezo hao walifanya usafi huo ikiwa ni sehemu ya uhamasishaji wa usafi wa Mazingira kwa watumishi walioshiriki mashindano hayo pamoja na Wananchi wa Mkoa wa Morogoro.

Imekuwa ni utaratibu wa kawaida kwa wanamichezo hao kuhamasisha usafi wa Mazingira kila mwaka kwenye mashindano ya SHIMMUTA huku wakienzi maono ya Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Immaculate Sware Semesi kuhakikisha Mazingira yanakuwa safi na yanaendelea kulindwa nchi nzima.

NEMC ilishiriki mashindano hayo ya SHIMMUTA 2025 ikiwa ni sehemu ya kuimarisha afya ya watumishi lakini pia kutumia fursa hiyo katika kutoa elimu kwa watumishi na Wananchi mkoani Morogoro kuhusiana na masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini.

Katika kuhakikisha elimu inafika kwa watu wa rika zote pia wanamichezo hao walitoa elimu ya Mazingira na kukabidhi vifaa vya kuzolea na kuhifadhia taka katika Shule ya Msingi Mwere ambapo wanamichezo hao walikuwa wanatumia viwanja vya shule hiyo kwa ajili ya mazoezi kipindi chote wakiwa kwenye mashindano hayo.

Mashindano ya SHIMMUTA 2025 yenye Kauli Mbiu isemayo "Uongozi Imara kwa Michezo Endelevu: Michezo ni Daraja la Afya, Amani, Umoja na Mshikamano wa Kitaifa" yalianza rasmi Novemba 23, 2025 na kufungwa rasmi Disemba 6, 2025 kwenye Uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro ambapo Mgeni Rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Kighoma Malima.

# NEMC YASHIRIKI MKUTANO WA SABA WA UMOJA WA MATAIFA KUHUSU MAZINGIRA

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilishiriki Mkutano wa Saba (07) wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira (07th United Nations Environment Assembly – UNEA-7) uliofanyika jijini Nairobi, Kenya kuanzia 08 hadi 12 Disemba 2025

Baadhi ya masuala yaliyojadiliwa katika Mkutano huu ni pamoja na Mazingira Asilia na Mabadiliko ya Tabianchi; Uchumi Mzunguko, kemikali, Taka na Uchafuzi wa Mazingira; Utawala na Sheria; na Bajeti.

Mkutano huu unaoongozwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Idara ya Mazingira, awali ulitanguliwa na mkutano wa maandalizi wa Kamati ya wawakilishi uliofanyika jijini hapo tarehe 01 hadi 05 Disemba 2025 ambapo wakuu wa nchi wanachama walitoa hotuba katika mkutano huo.

Zaidi ya NEMC, washiriki wengine ni pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Wakala wa Misitu (TFS) ambapo Kilele cha mkutano huu ni tarehe 11 na 12 Disemba 2025.




*Watumishi wa NEMC Walioshiriki Mkutano wa saba wa umoja wa mataifa kuhusu mazingira wakiwa katika picha ya pamoja, kushoto ni Meneja wa Kanda ya Nyanda za juu kusini Bw. Josiah Murunya, wapili ni Kaimu Meneja wa Mapitio ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Jamii (NEMC) Mha. Luhuvilo Mwamila, wa tatu ni Mwanasheria mwandamizi Bi. Mariam Mbaruku na wa kulia ni Meneja wa Kanda ya Morogoro/Rufiji Bw. Arnold Mapinduzi*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)

## Ni muhimu kuzingatia Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira ili kulinda afya na ustawi wa maendeleo ya Taifa letu. Linda vyanzo vya maji, panda miti na dhibiti taka.

**Dkt. Immaculate Sware Semesi**
**Mkurugenzi Mkuu - NEMC**

*#MazingiraYetuUhaiWetu. tuyatunze, yatutunze*

Wasiliana nasi


Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 inapiga marufuku shughuli zote za kibinadamu ndani ya umbali wa mita 60 kutoka kwenye vyanzo vya maji ili kulinda ubora wa maji pamoja na mifumo ya ikolojia ya maji.
Bw. Joannes Karungura
Mkurugenzi wa Huduma za Sheria - NEMC
#MazingiraYetuUhaiWetu. tuyatunze, yatutunze
Wasiliana nasi
nemctvtanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania


Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
Tukilinda vyanzo vya maji leo, tunalinda afya na Maisha ya kesho
Ni wajibu wa kila mmoja kuvilinda kwa maendeleo endelevu ya mazingira"
#MazingiraYetuUhaiWetu. tuyatunze, yatutunze
Wasiliana nasi
nemctvtanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania


Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
Kila tone la maji, kila mti na kila kiumbe ni sehemu ya mfumo wa ikolojia unaodumisha msingi na uhai wa Dunia.
"Tunza mazingira kwa kupanda miti, tupa taka mahali sahihi na hifadhi vyanzo vya maji ili kulinda mfumo wa Ikolojia"
#MazingiraYetuUhaiWetu. tuyatunze, yatutunze
Wasiliana nasi
nemctvtanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania


Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)
Usimamizi na uhifadhi wa misitu husaidia kupata hewa safi, maji, dawa na mazingira salama.
"Epuka ukataji miti holela, kwa ustawi wa vyanzo vya maji na mazingira."
#MazingiraYetuUhaiWetu. tuyatunze, yatutunze
Wasiliana nasi
nemctvtanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania
nemctanzania



*Wasiliana nasi;*


**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

Ghorofa ya 6, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF S.L.P 2724, Dodoma, Tanzania.

Simu: +255 713 608 930 Namba ya Bure: 0800 110 115

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz


#MazingiraYetuUhaiWetu


+255 680 400 400

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz